international
safeguarding
children in sport
working group

Ukingaji wa Kimataifa kwa Watoto katika Spoti

Orodha

Utangulizi	4
Fafanuzi	6
Maelezo ya Jumla ya Ukingaji	7
Malengo na Kanuni	10
Uchunguzi wa Majaribio	12
Hatua muhimu katika Safari ya Ukingaji	14
Njia ya Ukingaji 1: Kukuza Sera Yako	18
Njia ya Ukingaji 2: Taratibu za Kukabili Shughuli za Ukingaji	20
Njia ya Ukingaji 3: Ushauri na Usaidizi	22
Njia ya Ukingaji 4: Kupunguza Hatari kwa Watoto	24
Njia ya Ukingaji 5: Maelekezo kuhusu Tabia	26
Njia ya Ukingaji 6: Kuajiri, Kufunza na Kuwasiliana	28
Njia ya Ukingaji 7: Kufanya Kazi na Washirika	30
Njia ya Ukingaji 8: Kufuatilia na Kutathmini	32
Mashirika Anzilishi	34
Wanachama Waanzilishi	36

Utangulizi

Mamilioni ya watoto na vijana hushiriki katika shughuli za kispoti kila siku duniani kote. Kwa baadhi ya watoto hii ni kwa ajili ya kipekee ya starehe na kufurahia. Wengine hushiriki katika spoti kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa baadhi ya vijana spoti inaweza kuwa chaguo la taaluma yao ya siku za usoni, aidha kama wanariadha walio na kipawa, kama makocha au kama viongozi. Spoti inaweza pia kutumika kama nyenzo ya kuwaelekeza vijana dhidi ya tabia zilizo kinyume na jamii na jinai.

Watoto wana haki ya kushiriki katika spoti katika mazingira salama na ya kufurahisha. Haki zao zimo katika Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto.

Kwa miaka 15 iliyopita au zaidi waathiriwa wa aina zote za ghasia katika spoti wameanza kuwa na uwezo wa sauti zao kusikika na kujibiwa. Hapo awali kumekuwa na maswali machache kuhusu dhana kuwa spoti ndio juhudi tu bora kwa vijana. Hadi mwisho wa miaka ya 1990 na mapema miaka ya 2000 ni mashirika machache ya spoti yalikuwa yameweka mifumo na miundo ya kukabili malalamishi kuhusu tabia ya watu wakubwa na vijana wengine.

Sasa tunajua ya kutosha kutoka kwa utafiti na ushahidi ili kuwa wazi kuwa spoti kwa kawaida hautekelezwi kwa mtazamo kuhusu haki za watoto kuwa msingi au wakati mwingine hukosa kabisa kuangazia hatari kwa watoto, kusababisha mienendo ya mashirika ambayo hairuhusu mjadala kuhusu madhara na udhalimu (Brackenridge, Kay & Rhind, 2012).

Kuna hatari nyingi kwa watoto na vijana ambazo ni za kipekee kwa spoti kama vile ongezeko la hatari za aina zote za udhalimu kwa kikundi cha wanariadha wachanga. Spoti nyingi kwa miradi ya maendeleo hutolewa kwa watoto walio katika hatari kubwa wanaoweza kuathiriwa na ghasia na udhalimu katika maisha yao ya kila siku ambao kwao spoti inastahili kuwa mahali salama. Sisi wote tunastahili kutafuta kuhakikisha kuwa utoaji wa spoti kwa hawa vijana hufanyika katika mazingira salama.

Rasimu ya mkusanyiko wa Viwango (ambavyo sasa vinaitwa Njia ya ukingaji) zilikuzwa kwa ushirikiano wa mashirika yanayofanya kazi pamoja kwa Kongamano la Kupita Spoti katika London, 2012. Haya yalikuzwa zaidi kwa awamu ya majaribio ya kina ya miaka miwili ijayo. Tafsiri iliyokamilishwa ya Ukingaji ilizinduliwa katika Kupita Spoti mnamo Oktoba 2014. Waliweka msingi kwa mtazamo wa jumla wa kuhakikisha usalama wa watoto na ulindaji katika miktadha yote ya spoti kimataifa.

Fafanuzi

— Ukingaji hurejelea hatua tunazozichukua kuhakikisha kuwa watoto **WOTE** wako salama kutoka kwa madhara wanaposhiriki katika vyama na shughuli.

— Ulindaji wa watoto ni jumla ya shughuli zinazohitajika kwa watoto **MAHUSUSI** walio katika hatari ya/au wanaokabiliwa na udhalimu.

— Udhalimu hurejelea vitendo vyote vinavyofanywa au kutofanywa ambavyo hupelekea mtoto kupitia madhara.

— Dhara hurejelea athari hasi au athari kwa watoto wa vitendo hivyo.

— Ghasia hurejelea "aina zote za ghasia zinazoonekana na kiakili, jeraha na udhalimu, kutojali au utendeaji wa kutojali, kudhulumu au kunyanyasa, ukijumuisha udhalimu wa kimapenzi" (Kipengele 19 cha Mapatano ya UN kuhusu Haki za Mtoto)

Ukingaji wa Kimataifa

Hizi kingaji hulenga kuorodhesha vitu ambavyo vinastahili kuwekwa na shirika linalotoa shughuli za michezo kwa watoto na vijana. Kingaji hizi zinastahili kuonwa kama maelekezo, yanayoendeleza safari ya shirika kufikia ukingaji wa watoto badala ya kuwa mwisho wenyewe.

Huakisi maazimio ya kimataifa, Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto, sheria zinazofaa, mwongozo wa serikali, viwango vilivyopo vya kulinda na kukinga mtoto na utendaji bora. Wamejulishwa na utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Brunel na mitazamo ya mfiko anuwai kutoka kwa nchi mbalimbali na vikundi vya washika dau katika awamu ya kina ya majaribio.

Njia hizi za Ukingaji hizi huwakilisha utendaji bora wa jumla katika wakati maalum na zitakuwa zikibadilishwa mara kwa mara ili kuhakikisha zinaakisi maendeleo katika utendaji wa ukingaji.

Njia za ukingaji

Kingaji hizi 8 ni:

01 — Kukuza Sera Yako
02 — Taratibu za Kukabili Shughuli za Ukingaji
03 — Ushauri na Usaidizi
04 — Kupunguza Hatari kwa Watoto
05 — Maelekezo kuhusu Tabia
06 — Kuajiri, Kufunza na Kuwasiliana
07 — Kufanya kazi na Mashirika
08 — Kufuatilia na Kutathmini

Kingaji hizi zinalenga:

— Kusaidia kuunda mazingira salama ya kucheza ya watoto wanaposhiriki popote katika daraja yoyote.

— Kutoa alama teule ili kusaidia watoaji wa spoti na wafadhili kufanya maamuzi waliyoyawazia.

— Kukuza utendaji bora na kukabili utendaji ulio na madhara kwa watoto.

— Kutoa ufafanuzi kuhusu kukinga watoto kwa wote wanaoshughulika katika spoti.

Kingaji zimekitwa katika kanuni zifuatazo:

— Watoto wote wana haki ya kushiriki, kufurahia na kujikuza kupitia spoti, katika mazingira salama na ya kujumuisha, huru kutoka kwa aina zote za udhalimu, ghasia, kutojali na unyanyasaji.

— Watoto wana haki kuwa na sauti zao kusikika na kusikilizwa. Wanahitaji kujua nani wanayeweza kugeukia wanapokuwa na haja kuhusu kushirika katika spoti.

— Kila mmoja, mashirika na watu binafsi, watoaji wa huduma na wafadhili, wana jukumu la kusaidia utunzaji na ulinzi wa vijana.

— Mashirika yanayotoa shughuli za kispoti kwa watoto na vijana wana jukumu la utunzaji kwao.

— Kuna baadhi ya vigezo ambavyo huwaacha baadhi ya watoto wakiwa katika hatari kubwa ya kudhulumiwa, na hatua zinahitaji kuchukuliwa ili kutatua hili.

— Watoto wana haki ya kuhusishwa katika kuunda sera ya ukingaji na utendaji.

— Mashirika yanastahili kila wakati kutenda sawa zaidi na mahitaji ya watoto.

— Kila mtu ana haki ya kuhudumiwa kwa hadhi na heshima na kutobaguliwa dhidi ya jinsia, rangi, umri, kabila, uwezo, maelekezo ya mazingira ya kimapenzi, Imani, dini au muungano wa kisiasa.

— Michakato na shughuli kwa ajili ya kuunda, kukuza na kutekeleza vipimo vya ukingaji vinastahili kuwa wa kujumuisha.

Tafadhali kumbuka kuwa ijapokuwa kingaji hizi zimekuzwa kuhusiana na watoto (walio chini ya miaka 18) zinaweza pia kutoa mwongozo wa thamani kwa utendaji bora kuhusiana na vikundi vingine kama vile kwa watu wazima katika hatari.

Majaribio ya Kingaji

Idadi ya mashirika yaliyowakilishwa katika ari ya pamoja katika Kongamano la Kupita Mchezo 2012 walikubali kufanyia majaribio njia hizi za ukingaji pamoja na idadi ya mashirika zaidi kujitolea kuipa nguvu mtazamo ili kufanya spoti salama kwa watoto. Katika majaribio yote, uongozi wa ukingaji kutoka kwa mashirika haya ulishiriki katika Seti Bayana za Kufunza (VLS). VLS iliongozwa na mwanachama wa Kikundi cha Waasisi kilicho na ujuzi katika ukingaji wa watoto. Mashirika yalitengwa katika vikundi vidogo vya 6-8 kwa kuzingatia misheni, eneo na ukubwa. Hizi VLS vilikutana mtandaoni kila miezi miwili ili kujadili tajriba zao za kufanya kazi kuafikia Kingaji.

Majaribio ya Kingaji

Utafiti ulitekelezwa na Chuo Kikuu cha Brunel na mashirika haya 32. Data ilikusanywa kutoka kwa asili anuwai:

— Mahojiano na uongozi wa kukinga wa kila shirika.
— Majibu ya kila kipindi kutoka kwa viongozi wa VLS.
— Majibu yaliyokusanywa kutoka kwa mashirika ya majaribio katika Kupita Mchezo 2013 mjini Philadelphia.
— Uchunguzi kutoka kwa mtandao kwa washiriki kuhusiana na seti ya kingaji zilizofanyiwa marekebisho.

Kwa kuzingatia data hii, watafiti walifanya mapendekezo kwa Kikundi cha Waanzilishi. Tafsiri ya mwisho ya njia ya Ukingaji kisha iliundwa na kuzinduliwa katika Kupita Mchezo 2014. Maelezo zaidi kuhusu kila njia za ukingaji yametolewa hapa chini.

Hatua Muhimu katika Safari ya Kukinga

Hatua zifuatazo zitaielekeza safari yako kupitia katika kila Kingaji. Zitawezesha shirika kufikiria kuhusu mfumo wao wa sasa na kujulisha jitihada zao kuafikia usalama kwa watoto.

Mwongozo una hatua 5:

Hatua 01: Kujitayarisha kwa ajili ya safari
Kuinua fahamivu kuhusu haja ya kukinga watoto

Hatua 02: Tayarisha kutekeleza
Kuangazia ulipo sasa na kuzipa kipaumbele hatua zako zinazofuata

Hatua 03:
Kukuza njia zako za Ukingaji

Hatua 04:
Kutekeleza njia zako za Ukingaji

Hatua 05:
Utiaji ndani wa njia zako za ukingaji

Njia za Ukingaji

© UNICEF
UNI123577/Krzysiek

Kingaji 01
Kukuza Sera Yako

Nini — Shirika lolote linalotoa au lenye jukumu kwa shughuli za kispoti kwa watoto na vijana chini ya miaka 18 linastahili kuwa na sera ya ukingaji. Hii ni kauli ya kusudi ambayo inaonyesha kujitolea kuwakinga watoto wanaoshiriki katika spoti kutoka kwa madhara, na kutoa mwongozo ambao kwao taratibu zinakuzwa.

Mbona — Sera ya ukingaji inaweka wazi kwa wote kile kinachohitajika kuhusiana na kulinda watoto na vijana. Inasaidia kuunda mazingira salama na chanya kwa watoto na kuonyesha kuwa shirika linachukua jukumu lake la kutunza kwa makini. Inazingatia vigezo mahususi vinavyoweza kuwaacha watoto katika hatari kubwa.

Vigezo vya kufaulu

— Una sera ya ukingaji ambayo imeandikwa wazi na rahisi kuelewa.

— Sera inaeleza wazi wazi uelewa wako na fafanuzi wa aina zote za madhara.

— Sera inasheheni kujitolea kwa shirika lako kukinga watoto katika Nyanja zako zote za kazi.

— Sera ni wazi kuwa watoto wote wana haki sawa za kulindwa.

— Sera imeidhinishwa kirasmi na wahudumu katika daraja la juu la shirika lako.

— Wahudumu katika daraja la juu katika shirika wana jukumu la kufuatilia utekelezaji wa sera.

— Wahudumu wote, wanaojitolea, watunzaji na wawakilishi wengine wametia sahihi kwa sera.

— Shirika lako limeshauriana na watoto, wazazi/watunzaji na wahudumu kama sehemu ya kwanza ya kukuza na/au inayoendelea ya kudurusu sera yako.

Kingaji 02
Kukuza Mfumo wa Kukabili Haja za Ukingaji

Nini — Taratibu zinaeleza michakato ya operesheni zinazohitajika ili kutekeleza sera ya shirika na kuweka wazi mwongozo wa hatua-kwa-hatua kuhusu nini cha kufanywa katika mazingira tofauti. Zinaweka wazi nafasi na majukumu, na laini za mawasiliano. Mifumo bora inahitajika ambayo inasaidia njia ya kushughulikia malalamishi au haja na kusaidia waathiriwa wowote wa ghasia. Unastahili kujenga kwa mifumo iliyopo na kuelewa nafasi yako kuhusiana na mifumo na sheria ya kitaifa inayofaa.

Mbona — Kwa ukingaji kuwa bora, taratibu ziwe za kuaminika kwa watoto. Taratibu zinasaidia kuhakikisha ushughulikiaji wa haraka kwa haja kuhusu usalama wa watoto au kuwa salama. Pia zitakusaidia kuafikia na kutekeleza sheria na mwongozo. Ghasia dhidi ya watoto husikitisha na zinaweza kuwa ngumu kakabiliana nazo. Mashirika yana jukumu la kuhakikisha kuwa ushauri na msaada unawekwa ili kusaidia watu kutekeleza nafasi yao katika kukinga watoto.

Vigezo vya kufaulu

— Kuna taratibu wazi zilizowekwa ambazo zinatoa mwongozo wa hatua-kwa hatua kuhusu ni hatua ipi ya kuchukuliwa ikiwa kuna haja kuhusu usalama wa mtoto au kuwa salama, yote kutoka ndani au nje ya shirika.

— Shirika lako limeweka mipangilio ili kutoa msaada kwa watoto, wanaojitolea na wahudumu wakati wa na kufuata kitendo, tuhuma au lalamishi.

— Kuna mwanachama wa wahudumu katika shirika lako aliyetambuliwa kuchukua jukumu la kuongoza ukingaji.

— Shirika lako huwapa watoto na vijana ujumbe kuhusu haki zao na kuhusu nani watakayemwelekea ikiwa wana wasiwasi, katika mchakato ambao unawapa nguvu.

— Shirika lako limefanya ujumbe kupatikana kwa watoto na wazazi/watunzaji, kuhusu kile kinachoweza kutokea kufuatia ufichuzi, katika umbo na lugha ambayo inaweza kueleweka kwa urahisi.

— Shirika lako lina mchakato wa kushughulikia malalamishi katika njia ya haki na wazi, ambayo inajumuisha michakato ya ukataji rufaa.

— Matukio yote, tuhuma na malalamishi yamerekodiwa, kukaguliwa na kuhifadhiwa salama.

— Shirika lako limeshauriana na watoto, wazazi/watunzaji na wahudumu kama sehemu ya kwanza ya ukuzaji na/ au inayoendelea ya mfumo wako wa kushughulika.

Kingaji 03
Ushauri na Msaada

Nini — Mipangilio imefanywa ili kutoa ujumbe muhimu na msaada kwa wale walio na jukumu la kukinga watoto. Watoto na vijana wameshauriwa kuhusu ni wapi pa kupata usaidizi na msaada.

Mbona — Una jukumu la kuhakikisha ushauri na msaada unawekwa ili kusaidia watu kutekeleza nafasi zao katika kukinga watoto ili kwamba wajua ni nani wa kumgeukia kusaidiwa.

Vigezo vya kufaulu

— Mawasiliano yanawekwa katika kiwango cha kitaifa na/au chini na mashirika yanayofaa ya kuinda watoto, NGOs na vikundi vya jamii vinavyotoa msaada wa ulindaji wa watoto.

— Shirika lako linahakikisha kuwa wanachama wa wafanyi kazi walio na majukumu spesheli ya kuweka watoto salama wana mwingiliano na ushauri wa wataalamu, msaada na ujumbe.

— Watoto wanapewa ushauri na msaada kuhusu wao wenyewe na kila mmoja kuwa salama.

— Mfumo wako unatilia maanani kuwa watoto walio katika hatari kubwa (kwa mfano, walemavu) wanaweza kukabili vikwazo zaidi katika kupata usaidizi.

— Wazazi/watunzaji katika jamii pana wamepewa ujumbe, ushauri na msaada kuhusu kukinga watoto.

Kingaji 04
Kupunguza Hatari kwa Watoto

Nini — Vipimo vya kukadiria na kupunguza hatari kwa watoto.

Mbona — Baadhi ya watu, wanaofanya kazi au kutafuta kufanya kazi katika spoti katika hadhi ya kujitolea au kulipwa, ni hatari kwa watoto. Watoto pia wako katika hatari wanapowekwa katika mazingira yasiyofaa au wanapoulizwa kushiriki katika shughuli zisizofaa, ikijumuisha shughuli zisizofaa umri wao, kufunzwa zaidi na matarajio yasiyo halisi kwao. Inawezekana kupunguza hatari hizi kwa kuweka kingaji.

Vigezo vya kufaulu

— Ukadiriaji wa hatari unapatikana na kutekelezwa kwa shughuli, usafiri, vyumba na nafasi.

— Hatua zinachukuliwa kupunguza hatari zozote zilizotambuliwa kupitia kwa ukadiriaji wa hatari.

— Ikiwa hatari zimekadiriwa kuwa za umuhimu basi shughuli hasisongi mbele.

— Mafunzo yanapatikana ili kusaidia wahudumu na wanaojitolea kutambua hatari zaidi watoto wengine wanakabiliwa nazo, kwa sababu ya rangi yao, jinsia, umri, dini, ulemavu, maelekezo ya mazingira ya mapenzi, historia ya jamii au utamaduni.

Kingaji 05
Maelekezo kuhusu Tabia

Nini — Kanuni za utekelezaji za kueleza ni kipi kiwango cha tabia kinachokubalika na kuendeleza utendaji bora wa kisasa.

Mbona — Spoti ya watoto inastahili kufanywa katika mazingira salama, chanya na yanayotia moyo. Viwango vya tabia huweka alama teule ya ni kipi kinachokubalika kwa wote.

Vigezo vya kufaulu

— Shirika lako lina maelekezo yaliyoandikwa kwa tabia (kanuni za utekelezaji) yaliyo na kauli kuhusu kutendea watu kwa hadhi, heshima, kiwango cha hisi na kwa haki.

— Shirika lako lina maelekezo na matarajio kuhusu shughuli ambazo zinajumuisha muda uliotumika mbali na nyumbani, ikijumuisha kuweka watoto chini ya ulinzi wa wengine na kulala.

— Mashirika yanapohusika katika kuweka watoto chini ya ulinzi wa wengine, mikutano ya kila mara inafanywa pamoja na watoto ili kujadili tajriba zao.

— Shirika lako lina mwongozo kuhusu kufanya kazi na watoto walio na ulemavu.

— Shirika lako lina mwongozo kuhusu matumizi bora ya teknolojia ya habari na mtandao wa kijamii ili kuhakikisha kuwa watoto hawawekwi kwa hatari na kuwekwa katika hatari kubwa ya kunyanyaswa.

— Shirika lako lina mwongozo wa njia chanya za kushughulikia tabia ya watoto ambazo hazihusishi adhabu au aina yoyote ya kudunisha au kutendea kwa kushusha hadhi, na zinafaa kwa umri na jinsia.

— Shirika lako lina mwongozo kuhusu yanayotarajiwa na tabia ya kukubalika ya watoto kwa wengine, hasa watoto wengine (kwa mfano, patano la kujifunza)

— Kuna athari wazi kwa kutofuata maelekezo kuhusu tabia ambayo yanaunganishwa kwa taratibu za kinidhamu za shirika.

— Daraja la juu la shirika lina jukumu la kuhakikisha kuwa maelekezo yanatekelezwa.

— Shirika lako limeshauriana na watoto, wazazi/watunzaji na wahudumu kama sehemu ya kwanza ya kukuza na/au inayoendelea ya kudurusu maelekezo kuhusu tabia ya shirika lako.

Kingaji 06
Kuajiri, Kufunza na Kuwasiliana

Nini — Kuajiri wanachama wa wafanyi kazi wanaofaa, kubuni nafasi ili kukuza na kutunza stadi muhimu na kuwasiliana kuhusiana na kukinga.

Mbona — Kila anayetagusana na watoto ana nafasi ya kutekeleza katika ulinzi wao. Wanaweza tu kufanya hivyo kwa ujasiri na kuleta matokeo yanayohitajika ikiwa wanajua, wana uelewa muhimu wa, na nafasi za kukuza, kutenda na kutekeleza stadi muhimu. Mashirika yanayotoa shughuli za michezo kwa watoto wana jukumu la kutoa mafunzo na nafasi za ukuzaji kwa wahudumu na wanaojitolea.

Vigezo vya kufaulu

— Maelezo kuhusu kazi yanasheheni kauli kuhusu namna ya kuwatendea watu kwa hadhi, heshima, kiwango cha hisi na kwa haki.

— Mchakato wa kuajiri unajumuisha mahojiano, tabia/marejeleo ya ajira na kukagua historia kulingana na sheria ya wenyeji.

— Wahudumu wote, wanaojitolea na watu wengine wanaofaa wamefunzwa kuhusu kukinga na kulinda watoto, ikijumuisha namna ya kuripoti mashaka.

— Daraja la juu la shirika lina jukumu la kuangalia utekelezaji wa mafunzo

— Wahudumu wote, wanaojitolea na watu wote wanaofaa walio na majukumu spesheli wamepokea mafunzo kuhusu kukinga wanapata mafunzo ya ziada ya kila mara na msaada wa wataalamu.

— Shirika lako limeshauriana na watoto, wazazi/watunzaji na wahudumu kama sehemu ya kwanza ya ukuzaji na/au durusu inayoendelea kuhusu kuajiri, kufunza na ukuzaji wa shirika lako.

Kingaji 07
Kufanya kazi na Mashirika

Nini — Kuajiri wanachama wa wafanyi kazi wanaofaa, kubuni nafasi ili kukuza na kutunza stadi muhimu na kuwasiliana kuhusiana na kukinga.

Mbona — Idadi ya mashirika ya michezo wana nafasi katika kimkakati na uwasilishaji kuhusiana na watoto na vijana. Endapo ushirikiano wa mashirika, uanachama, ufadhili au uagizaji upo au unakuzwa pamoja na mashirika mengine, shirika linastahili kutumia ushawishi wake kuendeleza utekelezaji wa vipimo vya kukinga. Shirika linastahili kutoa au kuonyesha namna msaada na rasilmali kuhusiana na utekelezaji tosha wa vipimo vya kukinga. Shirika linastahili kuendeleza kikamilifu ukubaliano wa *Kingaji za Kimataifa kwa Watoto katika Mchezo.*

Vigezo vya kufaulu

— Shirika lako limefanya kazi na washirika/wanachama ili kuhakikisha kuwa kuna matarajio ya pamoja kuhusiana na ukingaji.

— Shirika lako limefanya kazi na washirika/wanachama ili kukubaliana mgawo wa mafunzo kuhusu kufanya spoti salama kwa watoto.

— Shirika lako limesambaza mwongozo ulioandikwa kuhusu utendaji bora wa sasa kuhusiana na kufanya kazi na watoto (kwa mfano kugawa Ukingaji wa Kimataifa kwa Watoto katika Spoti).

— Sera ya shirika lako ya kukinga inawasilisha sehemu muhimu ya makubaliano ya washirika/wanachama.

— Shirika lako huchapisha habari kuhusu sera yake kwa jamii, washirika na wanachama.

— Shirika lako linafanya kazi kuzihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kukinga watoto.

Kingaji 08
Usimamizi na Utathmini

Nini — Usimamizi unaoendelea wa kuafikia na wenye kuleta matokeo yanayofaa, unaohusisha vikundi vyote vinavyofaa.

Mbona — Mashirika yanahitaji kujua kama kukinga kunaleta matokeo yanayotakikana na wapi marekebisho na mabadiliko yanahitajika, au kutambua ruwaza za hatari.

Vigezo vya kufaulu

— Kuna mifumo imewekwa ili kufuatilia na kutathmini uletaji wa matokeo yanayohitajika wa shirika lako:

- Sera
- Mfumo wa kukabili haja za ukingaji
- Ushauri na msaada
- Mifumo ya kupunguza hatari kwa watoto
- Maelekezo kwa tabia
- Kuajiri, kufunza na kuwasiliana
- Kufanya kazi na mashirika ili kukinga watoto

— Daraja la juu la shirika lina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa kufuatilia na kutathmini.

— Shirika lako limeshauriana na watoto, wazazi/watunzaji na wahudumu kama sehemu ya kwanza ya ukuzaji na/au durusu inayoendelea ya mfumo wako wa kufuatilia na kutathmini.

Mashirika Anzilishi

AbleChildAfrica
ACER Brasil
Aquarius Spoti
Tume ya Spoti ya Australia
Blaze Sports America
Baraza la Uingereza
Chuo Kikuu cha Brown
Shirika la Kispoti ya Jumuiya ya Madola ya Brunei
Hazina ya Watoto Australia
Hazina ya Watoto Laos
Mstari wa Usaidizi wa Watoto wa Kimataifa
Makocha Kupita Mabara
Shirikisho la Michezo ya Jumuiya ya Madola
Jumuiya ya Madola Scotland Ltd
Baraza la Jumuiya ya Madola Cyprus
Watoto Viziwi Kimataifa
Wakfu wa Edusport
Shirikisho la Kimataifa la Netiboli
Isiqalo
Shirikisho la Ragbi Lao
Shirika la Tenisi
Magic Bus
Shirika la Spoti ya Jumuiya ya Madola Malta
Timu Manchester City FC
Timu Manchester United FC
Shirika la Spoti ya Jumuiya ya Madola Mauritius
Chuo Anuwai Moms TEAM/ SmartTeams
Moving the Goal Posts
Taasisi ya Spoti za Vijana (Singapore)
Kamati na Shirikisho la Michezo ya Olimpiki na Olimpiki ya walemavu ya Norway
Shirika la Taifa la Wanawake wa Michezo, Shughuli za Mwili na Burudani
Panathlon International
Chama cha Panathlon Sorocaba
Cheza na Funza
Haki ya Kucheza Thailand
Sadili Oval Sports Academy
Shirika la Kandanda la Scottish
Chama cha Michezo ya Jumuiya ya Madola - Ushelisheli
Skillshare International
Sport4Socialisation
Slum Soccer
Olympic Spesheli
Spirit of Soccer
Soccer without Borders
SportAccord
Sport Hampshire & IOW
Tackle Africa
UK Sport
UNNOSDP
Michezo na Utamaduni kwa Vipofu Urece
Uogeleaji USA
US Olympic Committee
World Sailing

Pass it Back, Vietnam
Mpiga-picha:
Phung Quang Binh

Imetayarishwa na Wanachama Waasisi:

Beyond Sport
Shirika la Spoti na Ukuzaji la Caribbean
Ulindaji wa watoto katika Kitengo cha Spoti
Comic Relief
Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola
International Inspiration
Kuweka Watoto Salama
Haki ya Kucheza
Swiss Academy for Development
UNICEF UK
UK Spoti
WomenWin

Imekuzwa kwa kuzingatia utafiti na:

Dkt Daniel Rhind
Prof. Celia Brackenridge
Prof. Tess Kay
Dkt Laura Hills na
Frank Owusu-Sekyere
(Brunel University, London)

Kwa msaada wa ukarimu kutoka kwa Wakfu ya Oak

Kwa habari Zaidi kuhusu kukuza kingaji katika shirika lako tafadhali tembelea:

http://www.sportanddev.org/en/toolkit/safeguarding_toolkit/

© International Inspiration
Rebecca Hearfield, 2012

© UNICEF/
UNI178925/Ramos

© 2016

Ukingaji wa
Kimataifa kwa
Watoto katika Spoti